

HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA



TANGAZO

UPANGISHAJI WA MAJENGO YA OFISI NA NYUMBA ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA ZILIZOPO MANISPAA YA SHINYANGA MWAKA WA FEDHA 2019/2020.

LGA/114/2020/2021/NC/BL/01

Tarehe 02.07.2020

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga anawatangazia Taasisi, Wafanyabiashara, Vikundi vilivyosajiliwa, Makampuni na Watu binafsi wenye uwezo wa kupanga au kuwekeza katika Majengo take yaliyop Manispaa ya Shinyanga kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021.


Majengo husika yana jumla ya vyumba 40 vinavyofaa kwa ajili ya matumizi ya ofisi mbalimbali na Nyumba 20 kwa ajili ya Makazi. Majengo hayo yapo katika eneo la Ushirika, mkabara na barabara kuu ya Shinyanga- Mwanza. Majengo yote yana Miundombinu ya Umeme, Maji, eneo la Maegesho ya Magari na eneo kubwa linaloweza kuendelezwa kwa ajili ya Uwekezaji zaidi.

MASHARTI YA UOMBAJI.

1. Mwombaji awe na shughuli inayotambulika kisheria.
2. Mwombaji asiwe na mgogoro wowote na Serikali.
3. Mwombaji awe na uwezo wa kulipa kodi ya pango kuanzia mwaka mmoja (1) na kuendelea.
4. Mwombaji atakayepata jengo atatakiwa alipe dhamana fedha taslimu zinazolingana na mawasilisho ya miezi miwili (2). Fedha hizi atarudishiwa baada ya Mkataba kuisha endapo atakuwa hadaiwi.
5. Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya maombi ya Shilingi Hamsini elfu tu (50,000/=) ambayo hairudishwi kwa kila ombi na kupewa stakabadhi pamoja na fomu ya maelekezo ya maombi katika ofisi ya **MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA.**
6. Mwombaji aambatishe uhalali wa kisheria (Power of attorney) wa mtu atakayehusika na zabuni hii.
7. Katika maombi yake Mwombaji aoneshe:-
 - a. Jina la Kampuni, Taasisi au Mtu binafsi.
 - b. Shughuli inayotayarajiwa kufanyika.
 - c. Jengo/Majengo anayo tarajia kupanga au kuwekeza.
 - d. Kiwango ambacho anaweza kulipa kwa mwezi .
8. Maombi yaandikwe kwa,

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P 113,
SHINYANGA .**

9. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 16/07/2020 saa 9:30 Mchana. Maombi yatakayochelewa hayatashughulikiwa.
10. Kwa Mwombaji atakayehitaji kuona Majengo awasiliane na Bw. Fredy Muhochi Simu Na. 0765 253 385 au Bi. Dianarose Kakulu, Simu Na. 0754411713.



Hoja N. Mahiba

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA.**